Voluntary Guidelines for Securing Sustainable Small-Scale Fisheries

in the Context of Food Security and Poverty Eradication

in Swahili (Tanzania)

Miongozo ya hiari kwa ajili ya Kupata Uhakika wa Uvuvi mdogo mdogo endelevu katika muktadha wa Usalama wa Chakula na Kuondoa Umaskini

YALIYOMO

VIFUPISHO NA AKRONIMI

CCA climate change adaptation
CEDAW Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination against Women
CSO Asasi za kiraia.
DRM Usimamizi wa hatari za majanga
EAF , Mbinu za mfumo ikolojia katika uvuvi.
HIV/AIDS human immunodeficiency virus Virusi vya kuzuiakinga ya Binadamu / acquired immunodeficiency syndrome/
ICESCR International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights
IGO intergovernmental organization Shirika la muungano wa Serikali
ILO International Labour Organization Shirika la Kazi Duniani
IMO International Maritime Organization Shirika la Kimataifa la mambo ya Bahari
IUU (fishing) illegal, unreported and unregulated (fishing) Uvuvi haramu, usioripotiwa na kudhibitiwa
MCS monitoring, control and surveillance Ufuatiliziaji, Udhibiti na Uangalizi
NGO non-governmental organization Asasi zisizo za Kiserikali
Rio+20 United Nations Conference on Sustainable Development (Rio+20) Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu.
The Code Code of Conduct for Responsible Fisheries (FAO)
UN United Nations Umoja wa Mataifa
UN DRIP United Nations Declaration on the Rights of Indigenous Peoples Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya haki za Wazawa.
UNFCCC United Nations Framework Convention on Climate Change:
WTO World Trade Organization Shirika la Biashara Duniani

DIBAJI

Miongozo hii ya Hiari kwa ajili ya Kupata Uhakika wa Uvuvi mdogo mdogo endelevu katika muktadha wa Usalama wa Chakula na Kuondoa Umaskini imeanzishwa kutoa nyongeza kwenye Kanuni ya Shirika la Umoja wa Nchi la Chakula na Kilimo ya mwenendo wa Uvuvi yakinifu ya mwaka1995. Ilianzishwa ili kutoa mwongozo wa ziada kuhusiana na uvuvi mdogo mdogo katika kusaidia kanuni za kiujumla na vipengele vya kanuni.

Kwa hiyo, miongozo ina nia ya kusaidia kujulikana, kutambulika na kukuza jukumu ambalo tayari ni la muhimu la uvuvi mdogo mdogo na kuchangia jitihada za kimataifa na kitaifa katika kutokomeza njaa na umaskini. Miongozo inasaidia uvuvi yakinifu na maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye, na kwa msisitizo juu ya wavuvi wadogo wadogo, wafanyakazi katika uvuvi na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na watu wanaoishi katika mazingira hatarishi na waliotengwa na kukuza mbinu za haki za binadamu.

Inasisitizwa kuwa Miongozo hii ni ya hiari, ina upeo wa kimataifa na kulenga mahitaji ya Nchi yanayoendelea.Uvuvi mdogo mdogo, unaojumuisha shughuli zote katika mlolongo wa thamani - kabla ya uvuvi, wakati wa uvuvi na baada ya uvuvi - unaofanywa na wanaume na wanawake, unachangia kwa kiasi kikubwa kwenye usalama wa chakula na lishe, kuondoa umaskini, usawa wa maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali. Uvuvi mdogo mdogo hutoa lishe bora kwa masoko ya ndani, kitaifa na kimataifa na kuzalisha mapato ya kusaidia uchumi wa wananchi na taifa.

Uvuvi mdogo mdogo huchangia nusu ya samaki wanaovuliwa ulimwenguni. Ukizingatia samaki waliovuliwa kwa ajili ya matumizi ya moja kwa moja ya binadamu, mchango unaochangiwa na sekta hii unaongezeka kwa theluthi mbili. Uvuvi kutoka katika maziwa na mito ni hasusani muhimu na uvuvi mdogo mdogo kwa ajili ya uzalishaji wa chakula ndio unaotawala katika sekta hii ndogo ya uvuvi.

Uvuvi mdogo mdogo huajiri zaidi ya asilimia 90 ya wavuvi na wafanyakazi katika uvuvi duniani, karibu nusu ya hao ni wanawake. Mbali na ajira kama wavuvi au wafanyakazi wa uvuvi wa kudumu au wa mda , uvuvi wa msimu au wa kipindi na shughuli zinazohusiana huwa ni nyongeza muhimu katika shughuli za kimaisha ya mamilioni ya watu. Shughuli hizi zinaweza kuwa za kawaida zanyongeza au kuwa za muhimu hasa katika nyakati za shida.

Wavuvi wadogo wadogo na wafanyakazi wa uvuvi wengi wamejiajiri na wanajishirikisha moja kwa moja katika utoaji wa chakula kwa ajili ya kaya na jamii zao na vile vile kufanya kazi katika uvuvi wa kibiashara, usindikaji na masoko. Uvuvi na shughuli zinazohusiana mara nyingi huimarisha uchumi wa ndani wa jamii katika maeneo ya pwani, maziwa na kandokando ya mto na ni injini, inayoeneza athari katika sekta nyingine.

Uvuvi mdogo mdogo unawakilisha sekta ndogo yenye watu mbalimbali na inayobadilika badilika ambayo mara nyingi inajulikana kuwa na sifa ya kuhama hama kwa msimu. Sifa sahihi ya sekata ndogo hii hutofautiana kutegemea na eneo, na ni ukweli kwamba , uvuvi mdogo mdogo huwa umejikita sana katika jamii, kuonyesha mara nyingi uhusiano wa kihistoria na rasilimali za uvuvi zilizo karibu, mila na maadili, na husaidia mshikamano wa jamii.

Kwa wavuvi wadogo wadogo na wafanyakazi katika sekta ya uvuvi wengi, uvuvi unawakilisha njia ya maisha na sekta hii ndogo inajumuisha mchanganyiko na utajiri wa kiutamaduni ambao ni wa umuhimu ulimwenguni.

Wavuvi wadogo wadogo wengi, wafanyakazi katika sekta ya uvuvi na jamii zao - pamoja na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi na waliotengwa - ni tegemezi moja kwa moja juu ya upatikanaji wa rasilimali za uvuvi na ardhi. Haki za umiliki wa ardhi katika ukanda wa pwani na fukwe ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha na kurahisisha ufikaji kwenye uvuvi, kwa ajili ya shughuli ambatanishi (ikiwa ni pamoja na usindikaji na masoko), na kwa ajili ya makazi na misaada mingine ya kimaisha. Afya ya ikolojia ya majini na bionuai husika ni msingi muhimu kwa maisha yao na kwa uwezo wa sekta hii ndogo kuchangia kwa ujumla ustawi wao.

Pamoja na umuhimu wake, jamii nyingi za wavuvi wadogo wadog huendelea kutengwa , na mchango wao kwa usalama wa chakula na lishe, kuondoa umaskini, usawa wa maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali- ambapo unawafaidisha wao na hao wengine – hauonekani kikamilifu.Kwa urefu 'rasilimali za uvuvi' katika waraka huu inashughulikia wote wanaoishi kutegemea rasilimali za majini (mwani, samakigamba, nk katika wawili baharini na freshwaters) kwamba ni kawaida chini ya kuvuna
Kupata na kuongeza mchango wa uvuvi mdogo mdogo unakabiliwa na changamoto nyingi na vikwazo. Maendeleo ya sekta ya uvuvi katika kipindi cha miongo 3-4 mara nyingi yamepelekea kwenye matumizi yaliyokithiri ya rasilimali na vitisho dhidi ya makazi ya viumbe na mfumo wa ikolojia duniani.

Vitendo vya kimila kwa ajili ya mgao na kugawana manufaa ya rasilimali katika uvuvi mdogo mdogo, ambao umekuwepo kwa vizazi vingi, umebadilishwa kutokana na mifumo isiyo shirikishi na wakati mwengine utaratibu wa usimamizi wa uvuvi wa serikali kuu , mabadiliko ya haraka ya maendeleo ya teknolojia na mabadiliko ya idadi ya watu.

Jamii za wavuvi wadogo wadogo pia kwa kawaida inakabiliwa na mahusiano yasiyo sawa ya nguvu za madaraka. Katika maeneo mengi, migogoro na uvuvi mkubwa ni tatizo , na kuna ongezeko la kutegemeana au ushindani kati ya uvuvi mdogo mdogo na sekta nyingine.

Sekta hizi nyingine mara nyingi zinaweza kuwa na nguvu na ushawishi wa kisiasa au kiuchumi, hizi ni pamoja na: utalii, ufugaji wa viumbe vya majini, kilimo, nishati, uchimbaji madini, viwanda na uendelezaji wa miundombinu.

Umasikini unapokuwepo katika jamii za wavuvi wadogo wadogo, una asili yenye upana mchanganyiko na si tu unasababishwa na kipato cha chini lakini pia unatokana na mambo ambayo yanazorotesha kufurahia haki za binadamu ikiwa ni pamoja na haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Jamii za wavuvi wadogo wadogo kwa kawaida ziko katika maeneo ya mbali na huwa na ufinyu au kutokuwa na uwezo wa kuyafikia masoko, na inaweza kuwa na ufikiaji duni wa huduma za afya, elimu na huduma nyingine za kijamii.

Sifa nyingine ni pamoja na viwango vya chini vya elimu rasmi, kuwepo kwa matatizo ya kiafya (mara nyingi ikiwa ni pamoja na matukio ya VVU / UKIMWI yaliyo juu ya wastani) na miundo duni ya kiutawala. Fursa zilizopo ni ndogo, kwa vile jamii za wavuvi wadogo wadogo zinakabiliwa na ukosefu wa maisha mbadala, ajira kwa vijana, mazingira ya kazi mabaya na yasiyo salama, kazi ya kulazimishwa, na ajira kwa watoto.

Uchafuzi , uharibifu wa mazingira, na athari za mabadiliko ya tabia nchi na majanga ya asili na yanayosababishwa na binadamu, huongeza matishio yanayozikabili jamii za wavuvi wadogo wadogo. Mambo haya yote hufanya iwe vigumu kwa wavuvi wadogo wadogo na wafanyakazi katika sekata ya uvuvi sauti zao kusikika, kutetea haki zao za kibinadamu na haki za umiliki, na kupata uhakika wa matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi ambazo wao huzitegemea.

Miongozo hii imetengenezwa kupitia mchakato shirikishi na wamashauriano, uliojumuisha wawakilishi wa jamii za wavuvi wadogo wadogo , asasi za kiraia (CSOs), serikali, mashirika ya kikanda na wadau wengine.

Kisha Wataalamu wa Ushauri Ufundi wa Shirika la Umoja wa Nchi wa Chakula na Kilimo walifanya mapitio . Wao waliyachukua kwa upana fikra/mapendekezo muhimu na kanuni, ikiwa ni pamoja na usawa na kutobaguliwa, ushiriki na ushirikishwaji, uwajibikaji na utawala wa sheria, na kanuni kwamba haki za binadamu ni za ulimwegu mzima, hazigawanyiki, zinahusiana na kutegemeana. Miongozo inaendana na inakuza viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

Miongozo hii ni nyongeza ya kanuni na vyombo vyake vinavyohusiana. Pia inazingatia miongozo ya kitaalamu, kama vile Miongozo ya Kitaalamu ya Uvuvi Yakinifu No. 10 "Kuongezeka kwa Mchango wa uvuvi mdogo mdogo katika Usalama wa Chakula na Kupunguza Umaskini ", na pia vyombo vingine vya hiari vya kimataifa, kama vile Mwongozo wa hiari juu ya Utawala wa Umiliki wa Ardhi, Uvuvi na Misitu katika muktadha wa Taifa wa Usalama wa Chakula (Miongozo ya Umiliki) na miongozo ya Hiari katika kusaidia kufikiwa kwa Haki ya Chakula cha kutosha katika muktadha wa Taifa wa Usalama wa Chakula (Miongozo ya Haki ya Chakula), kama itakavyotumika. Taifa na wadau wengine wanahimizwa pia kufanya mapitio ya miongozo hii mingine, kama vile vyombo vya kimataifa na kikanda, ili kuunganisha kikamilifu majukumu husika, ahadi ya hiari na miongozo iliyopo.

SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI

1. **MADHUMUNI**

1.1 Madhumuni ya Miongozo hizi ni: a) Kuongeza mchango wa uvuvi mdogo mdogo katika usalama wa chakula na lishe ulimwenguni na kusaidia kufikiwa kwa haki ya chakula cha kutosha, b) Kuchangia kuendeleza jamii za wavuvi wadogo wadogo kwa usawa na kuondoa umaskini na kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi ya wavuvi na wafanyakazi katka sekta ya uvuvi katika muktadha wa usimamizi endelevu wa uvuvi. c) Kufikia matumizi endelevu, umakini na kuwajibika katika usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi sambamba na Kanuni za Maadili kwa ajili ya Uvuvi yakinifu na vyombo vinavyohusiana , d) kukuza mchango wa uvuvi mdogo mdogo katika uchumi, jamii na mazingira endelevu ya baadaye kwa ajili ya dunia na watu wake, e) kutoa mwongozo ambao unaweza kufikiliwa na nchi na wadau kwa ajili ya uanzishwaji na utekelezaji wa mfumo wa ikolojia rafiki na sera shirikishi, mikakati na mifumo ya kisheria kwa ajili ya kukuza uvuvi mdogo mdogo yakinifu na endelevu,
f) kuongeza uelewa wa umma na kukuza maendeleo ya elimu kuhusu utamaduni, jukumu, mchango na uwezo wa uvuvi mdogo mdogo, kwa kuzingatia maarifa ya kale na jadi, na vikwazo na fursa vinavyohusiana.

1.2 Malengo haya lazima yafikiwe kupitia ukuzwaji wa mbinu za haki za binadamu, na kuziwezesha jamii za wavuvi wadogo wadogo, ikiwa ni pamoja na wanaume na wanawake, kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi, na kuchukua majukumu ya matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, na kuweka mkazo juu ya mahitaji ya nchi zinazoendelea na kwa manufaa ya makundi yaliyo katika hali hatarishi na yaliyotengwa.

2. **ASILI NA WIGO**

2.1 Hizi Miongozo kwa asili ni ya hiari. Miongozo inapaswa kutumika kwa uvuvi mdogo mdogo katika muktadha wote wote, iwe na wigo wa ulimwengu wote lakini ikiwa imelenga mahsusi juu ya mahitaji ya nchi zinazoendelea.

2.2 Miongozo hizi zinafaa kwa uvuvi mdogo mdogo katika bahari, maziwa na mito, kwa maana ya wanaume na wanawake wanaofanya shughuli mbalimbali kwenye mlolongo wa thamani, na shughuli za kabla na baada ya uvuvi. Uhusiano muhimu kati ya uvuvi mdogo mdogo na ufugaji wa viumbe vya majini unatambuliwa, lakini Miongozo hii hasa imelenga zaidi kwenye shuguli za uvuvi wa samaki.

2.3 Miongozo ni kwa wanachama na wasiyo wanachama wa Shirika la Umoja wa Nchi la Chakula na Kilimo (FAO) na, katika ngazi zote za nchi , ikiwa ni pamoja na kanda ndogo, kanda, kimataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa (IGOs) na wanaohusika katika sekata ya uvuvi mdogo mdogo (wavuvi, wafanyakazi katika sekta ya uvuvi, jamii zao, mamlaka za kijadi na kimila, mashirika ya kitaalamu na asasi za kiraia). Pia imelenga taaasisi za utafiti na za kitaaluma, sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na wengine wote

wanaohusika na sekta ya uvuvi, maendeleo ya pwani na vijijini na matumizi ya mazingira ya maji

2.4 Miongozo inatambua tofauti kubwa iliyopo kwenye uvuvi mdogo mdogo na kwamba hakuna ufafanuzi mmoja uliokubalika wa sekta hii ndogo. Kwa hiyo, miongozo haina viwango vya ufafanuzi juu ya uvuvi mdogo mdogo wala jinsi miongozo inapaswa kutumika katika mazingira ya kitaifa. Miongozo hii inafaa hasa kwa uvuvi mdog mdogo na wavuvi walio katika mazingira hatarishi. Ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya miongozo, ni muhimu kuhakikisha waendeshaji gani na shughuli zipi zinazofikiriwa kuwa ni ndogo ndogo, na kutambua makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi na waliotengwa wanaohitaji uangalifu mkubwa. Hii lazima ifanyike katika ngazi ya kanda , kanda ndogo au ngazi ya taifa na kulingana na mazingira fulani ambayo itatumika. Nchi inapaswa kuhakikisha kwamba utambuzi na matumizi yanaongozwa kwa ushirikishi, mashauriano, ya ngazi zote na michakato yenye malengo ili sauti za wanawake na wanaume zisikike. Pande zote zinapaswa kuunga mkono na kushiriki, katika michakato hizo kama inafaa na muhimu,.

2.5 Miongozo hii lazima kufasiriwa na kutumiwa kwa mujibu wa mifumo ya kisheria ya nchi na taasisi zake.

3. KANUNI ZA KUONGOZA

3.1 Miongozo hii inatokana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, viwango na matendo ya uvuvi yakinifu na maendeleo endelevu kwa mujibu wa matokeo ya waraka wa Mkutano wa Umoja wa Nchi juu ya Maendeleo Endelevu (Rio + 20) 'Hali ya baadaye tunayotaka', Kanuni na vyombo vingine husika, kutoa umakini hasa kwa makundi yaliyo katika hali hatarishi na yaliyotengwa na haja ya kusaidia utambuzi wa haki ya chakula cha kutosha.

1. **Haki za Binadamu na hadhi**: kutambua hadhi ya asili na usawa na haki za binadamu za watu wote zisizoegemea upande wowote, pande zote zinapaswa kutambua, kuheshimu, kukuza na kulinda kanuni za haki za binadamu na matumizi yake kwa jamii tegemezi kwenye uvuvi mdogo mdogo , kama ilivyoainishwa na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu: umoja na kutoegemea pande yeyote, kutokugawanyika, kutegemeana na kuhusiana, kutokubaguana na usawa; ushiriki na ushirikishwaji, uwajibikaji na utawala wa sheria. Nchi zinapaswa kuheshimu na kulinda haki za watetezi wa haki za binadamu katika kazi zao juu ya uvuvi mdogo mdogo.

Asasi zisizo za serikali ikiwa ni pamoja na makampuni ya biashara yanayohusika na au kuathiri uvuvi mdogo mdogo wana wajibu wa kuheshimu haki za binadamu. Nchi zinapaswa kusimamia wigo wa shughuli kuhusiana na uvuvi mdogo mdogo wa asasi zisizo za serikali kuhakikisha zinafuata viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

2. Kuheshimu tamaduni: kutambua na kuheshimu aina zilizopo za shirika, maarifa na matendo ya kijadi na kiutamaduni wa jamii za wavuvi wadogo wadogo, ikiwa ni pamoja na wenyeji na

makabila madogo kuhamasisha uongozi wa wanawake na kwa kuzingatia ibara. 5 ya Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW).

3. Kutokubagua : kukuza uvuvi mdogo mdogo na kuondoa kila aina ya ubaguzi katika sera na katika matendo.

4. Usawa wa kijinsia na mgawanyo ni msingi katika maendeleo yoyote. Kwa kutambua majukumu muhimu ya wanawake katika uvuvi mdogo mdogo, haki na fursa sawa lazima kukuzwa.

5. Mgawanyo na usawa: kukuza kuhukumiwa na kutendewa kuliko sawa – vyote katika sheria na matendo – kwa watu wote, ikiwa ni pamoja na haki sawa ya kufurahia haki zote za binadamu. Wakati huo huo, kukiri kuwepo kwa tofauti kati ya wanawake na wanaume na hatua maalum kuchukuliwa ili kuharakisha uhalisi wa usawa, yaani kutumia upendeleo unapotakiwa ili kufikia matokeo sawa, hasa kwa makundi yaliyo katika hali hatarishi na yaliyotengwa.

6.Ushauri na ushiriki: kuhakikisha ushiriki wa jamii za wavuvi wadogo wadogo wa kufahamisha, unaofanyakazi, ulio huru , wenye ufanisi na wenye maana , ikiwa ni pamoja na wazawa, kwa kuzingatia Azimio la Umoja wa Nchi juu ya Haki za Wazawa (UN DRIP) katika michakato yote ya maamuzi kuhusiana na rasilimali za uvuvi na maeneo ambapo uvuvi wadogo wadogo unakofanyika pamoja na maeneo ya ardhi yaliyo jirani , na kutilia maanani madaraka yasiyo sawa kati ya pande mbalimbali. Hii ni pamoja na mrejesho na msaada kwa wale ambao watakaoathirika na maamuzi kabla ya hatua zinazochukuliwa, na kuitikia michango yao.

7. Utawala wa sheria: kupitisha mbinu zinazoengemea kwenye utawala kwa ajili ya uvuvi mdogo mdogo kupitia sheria ambazo zimetangazwa kwa upana na katika lugha inayotumika , na inatumika kwa wote, na kutekelezwa kwa usawa na yenye kuamuliwa bila kutegemea upande wowote , na kwamba inaendana na majukumu yaliyopo chini ya sheria ya nchi na ya kimataifa, na kwa kuheshimu ahadi ya hiari chini ya vyombo husika vya kikanda na kimataifa.

8. Uwazi: kufafanua kwa wazi na kutangaza kwa upana sera, sheria na taratibu katika lugha inayotumika, na kutangaza kwa upana maamuzi katika lugha inayotumika na katika muundo unaopatikana kwa wote.

9. Uwajibikaji: kuwajibisha watu binafsi, mashirika ya umma na yasiyo ya kiserikali kwa matendo yao na maamuzi kulingana na kanuni za utawala wa sheria.

10. Uchumi, kijamii na mazingira endelevu: kutumia mbinu za tahadhari na usimamizi wa hatari ili kulinda dhidi ya matokeo yasiyotakikana, ikiwa ni pamoja na matumizi kupita kiasi ya rasilimali za uvuvi na athari hasi za mazingira, kijamii na kiuchumi .

11. Mbinu kamilifu na kijumla : kutambua kuwa mbinu ya mfumo wa ekolojia kuhusu uvuvi (EAF) kama ni kanuni muhimu ya kuongoza, kuungana na dhana kabambe na endelevu ya

maeneo yote ya mfumo ekolojia pamoja na shughuli za maisha ya jamii za wavuvi wadogo wadogo, na kuhakikisha uratibu wa sekta mtambuka kwa vile uvuvi mdogo mdogo una uhusiano wa karibu na kutegemea sekta nyingine nyingi....

12. Kuwajibika juu ya Jamii: kukuza mshikamano wa jamii na wajibu wa pamoja . Kukuza mazingira ambayo yanakuza ushirikiano wa wadau .

13. Uwezekano kijamii na kiuchumi yakinifu: kuhakikisha kuwa sera, mikakati, mipango na hatua kwa ajili ya kuboresha utawala bora wa uvuvi mdogo mdogo na maendeleo inakuwa na mantiki kijamii na kiuchumi. Inapaswa kupata taarifa za mazingira yaliyopo, inawezekana kutekelezeka na kutumiwa katika mabadiliko ya hali, na lazima isaidie jamii kuhimili mabadiliko.

4. MAHUSIANO NA VYOMBO VINGINE VYA KIMATAIFA.

4.1 Miongozo hii ni lazima kufasiriwa na kutumiwa sambamba na haki na wajibu zilizopo chini ya sheria ya kitaifa na kimataifa na kwa kuzingatia ahadi ya hiari chini ya vyombo husika vya kikanda na kimataifa. Ni nyongeza na inasaidia juhudi za kitaifa, kikanda na kimataifa ambazo zinashughulikia haki za binadamu, uvuvi yakinifu na maendeleo endelevu. Miongozo imetengenezwa kama nyongeza za kanuni na kusaidia uvuvi yakinifu na matumizi endelevu ya rasilimali kwa mujibu wa chombo hiki.

4.2 Hakuna katika mwongozo huu ambacho kitasomeka kama ni kikwazo au kudhoofisha haki yoyote au majukumu ambayo nchi inaweza kuwa chini ya sheria za kimataifa. Miongozo hii inaweza kutumika kuongoza marekebisho na kuhamasisha nyongeza mpya au nyongeza za sheria na vipengele vyake.

SEHEMU YA 2: UVUVI YAKINIFU NA MAENDELEO ENDELEVU.

5. UTAWALA WA MILIKI KATIKA UVUVI MDOGO MDOGO NA USIMAMIZI WA RASILIMALI.

5.1 Hii Miongozo inatambua haja ya uwajibikaji katika matumizi endelevu ya bionuai ya majini na maliasili ili kukidhi maendeleo na mahitaji ya kimazingira ya sasa na vizazi vijavyo. Jamii za wavuvi mdogo mdogo zinahitaji kuwa na haki za umiliki kwenye rasilimali ambazo ni msingi kwa ajili ya ustawi wa kijamii na kiutamaduni , maisha na maendeleo yao endelevu. Miongozo inasaidia mgawanyo sawa wa manufaa utokanao na usimamizi yakinifu wa uvuvi na mfumo ikolojia , kutunuku wavuvi wadogo wadogo na wafanyakazi katika sekta ya uvuvi , wanaume na wanawake kwa pamoja.

5A. Utawala wa Kuwajibika katika Umiliki

5.2 Wahusika wote wanapaswa kutambua kwamba utawala yakinifu wa miliki za ardhi, uvuvi na misitu unaotumika katika uvuvi mdogo mdogo ni muhimu kwa ajili ya kuzifikia haki za binadamu, usalama wa chakula, kuondoa umaskini, shughuli za kimaisha endelevu, utulivu wa kijamii, makazi salama, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya vijijini na ya kijamii.

5.3 Nchi , kwa mujibu wa sheria zao, zinapaswa kuhakikisha kuwa wavuvi wadogo wadogo, wafanyakazi katika sekta ya uvuvi na jamii zao, wanapata haki za kumiliki rasilimali za uvuvi (baharini na bara), zilizo sawa, sahihi kijamii na kiutamaduni kwenye maeneo yao ya uvuvi mdogo mdogo na ardhi jirani , na kipaumbele maalum kupewa kwa wanawake juu ya haki za umiliki.

5.4 Wahusika wote , kwa mujibu wa sheria zao, wanapaswa kutambua, kuheshimu na kulinda aina zote za haki miliki, kwa kuzingatia, inapostahiki, haki za kimila, juu ya rasilimali za majini na maeneo ya ardhi na sehemu za uvuvi mdogo mdogo zinazotumika na jamii ya wavuvi wadogo wadogo. Inapobidi , ili kulinda aina mbalimbali za haki za umiliki, ni lazima sheria zitolewe.

Nchi zinapaswa kuchukua hatua mwafaka kutambua, kuweka rekodi na kuheshimu wamiliki halali na haki zao. Taratibu na vitendo vya wenyeji ikiwa ni pamoja na mila au vinginevyo, upendeleo wa kuzifikia rasilimali za uvuvi na ardhi kwa jumuiya za wavuvi wadogo wadogo ikiwa ni pamoja na wazawa na makabila madogo zinapaswa kutambuliwa, kuheshimiwa na kulindwa, kwa njia ambazo ni sambamba na sheria ya kimataifa ya haki za binadamu. UN DRIP na Azimio kuhusu Haki za Watu walio katika Taifa au kabila, dini pia zizingatiwe inavyostahiki. Inapotokea mabadiliko ya katiba au kisheria ya kuimarisha haki za wanawake yanagongana na mila na desturi, inabidi pande zote kushirikiana ili kuweza kuyaingiza mabadiliko hayo katika mifumo ya umiliki wa kimila.

5.5 Nchi ni budi zitambue nafasi ya jumuiya za wavuvi wadogo wadogo na wazawa kurejesha, kuhifadhi, kulinda na kusimamia kwa pamoja mfumo ekolojia wa majini na pwani

5.6 Iwapo Nchi ndio zinamiliki au kudhibiti maji (ikiwa ni pamoja na rasilimali za uvuvi) na rasilimali ardhi,zinapaswa kuamua matumizi na haki miliki za rasilimali hizi kwa kuzingatia, pamoja na mambo mengine, malengo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira. Nchi lazima, inapohitajika , kutambua na kulinda rasilimali za umma zinazotumika na kusimamiwa kwa pamoja, hasa na jamii za wavuvi wadogo wadogo

5.7 Ukichukulia Kifungu. 6.18 ya Kanuni, Nchi zinapaswa pale inapobidi kutoa upendeleo kwa uvuvi mdogo mdogo wa kuvua samaki katika maji yaliyo chini ya mamlaka ya taifa, kwa muono wa kufikia usawa wa matokeo kwa makundi mbalimbali ya watu, hasa makundi ya walio katika hali hatarishi. Inapobidi , hatua maalum, pamoja na mambo mengine uundwaji na utekelezaji wa kanda maalum kwa ajili ya uvuvi mdogo mdogo inabidi kufikiriwa. Uvuvi mdogo mdogo hauna budi kuzingatiwa kabla ya kuingia mikataba ya upatikanaji wa rasilimali na Nchi nyingine na wahusika mwingine.

5.8 Nchi zinapaswa kuchukua hatua ili kuwezesha upatikanaji uliosawa wa rasilimali za uvuvi kwa jamii za wavuvi wadogo wadogo, ikiwa ni pamoja na kama inafaa, mageuzi ya mgawanyo , kwa kuzingatia masharti ya Muongozo wa Hiari juu Majukumu ya Utawala wa Umiliki Ardhi, Uvuvi na Misitu katika Muktadha wa Usalama wa Taifa ya Chakula

5.9 Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa jamii za wavuvi wadogo wadogo hawahamishwi kiholela na kwamba haki za umiliki halali kwa vyovyote vile hazifutwi au kuingiliwa. Nchi inapaswa kutambua kuwa ushindani kutoka kwa watumiaji wengine unaongezeka katika maeneo ya uvuvi mdogo mdogo na kwamba jamii ya wavuvi wadogo wadogo , hasa makundi yaliyo katika hali hatarishi na yaliyotengwa , mara nyingi ni makundi dhaifu katika migogoro na sekta nyingine na yanahitaji msaada maalum kama maisha yao yatatishiwa na maendeleo na shughuli za sekta nyingine *2 Neno ' Haki miliki ' hutumiwa kwa mujibu wa Muongozo wa Hiari juu Majukumu ya Utawala wa Umiliki Ardhi, Uvuvi na Misitu katika Muktadha wa Usalama wa Taifa ya Chakula*

5.10 Nchi na vyama vingine lazima, kabla ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa inaweza kuathiri jamii za wavuvi wadogo wadogo, zifikirie athari za kijamii, kiuchumi na kimazingira kwa kufanyika uchunguzi wa athari, na yafanyike mashauriano fanisi na yenye maana na jumuiya hizo, kwa mujibu wa sheria ya nchi

5.11. Nchi zinapaswa kuzipa jamii za wavuvi wadogo wadogo na watu binafsi, ikiwa ni pamoja na watu walio katika hali hatarishi na waliotengwa, kwa wakati, gharama nafuu na ufanisi kupitia mahakama huru na vyombo vya kiutawala , njia ya kutatua migogoro juu ya haki za umiliki kwa mujibu wa sheria za kitaifa, ikiwa ni pamoja na njia mbadala ya kutatua migogoro hiyo, na zinapaswa kutoa tiba zenye ufanisi ambazo ni pamoja na haki ya kukata rufaa, kama inafaa. Tiba hizo zinatakiwa kutekelezwa haraka kwa mujibu wa sheria za nchi na inaweza kuwa ni pamoja na kurekebishwa, indemnity, fidia ya haki na reparation

5.12 Nchi zinapaswa kujitahidi kurejesha kwa jamii za wavuvi wadogo wadogo ambazo zimehamishwa makazi yao kutokana na majanga ya asili na / au vita, ufikaji katika maeneo ya uvuvi wa jadi na maeneo ya pwani kwa kuzingatia uendelevu wa rasilimali za uvuvi. Nchi zianzishe utaratibu wa kuzisaidia jamii za wavuvi walioathirika na ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu ili ziweze kujenga maisha na shughuli za kimaisha . Hatua hiyo ni pamoja na uondoaji wa aina yoyote ile ya ubaguzi dhidi ya wanawake katika taratibu za umiliki wakati wa majanga ya asili na / au vita.

5 B. Usimamizi endelevu wa rasilimali

5.13 Nchi na wote wanoshiriki katika usimamizi wa uvuvi wanapaswa kuchukua hatua kwa ajili ya hifadhi ya muda mrefu na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kupata msingi wa ikolojia kwa ajili ya uzalishaji wa chakula. Wanapaswa kukuza na kutekeleza mifumo sahihi ya usimamizi, sambamba na majukumu yao chini ya sheria zilizopo za nchi na kimataifa na ahadi za hiari, ikiwa ni pamoja na Kanuni, zinazotambua mahitaji na fursa ya uvuvi wadogo wadogo

5.14 Wahusika wote ni lazima kutambua kwamba haki na majukumu huja pamoja; haki za umiliki huwiana na majukumu, na husaidia uhifadhi wa muda mrefu na matumizi endelevu ya rasilimali na utengenezwaji wa msingi wa ikolojia kwa ajili ya uzalishaji wa chakula. Wavuvi wadogo wadogo wanapaswa kutumia njia za uvuvi ambao unapunguza madhara kwa mazingira ya majini na spishi husika na kusaidia uendelevu wa rasilimali.

5.15 Nchi inapaswa kuwezesha, kufundisha na kusaidia jamii za wavuvi wadogo wadogo kushiriki na kuchukua jukumu , kwa kuzingatia haki zao halali za mfumo wa umiliki , usimamizi wa rasilimali ambazo wao huzitegemea kwa ajili ya ustawi wao na kwamba kiasili,hutumiwa kwa ajili ya maisha yao. Ipasavyo, Nchi zinapaswa kushirikisha jumuiya za wavuvi wadogo wadogo - na kipaumbele kikiwa kwa ushiriki sawa wa wanawake, makundi yaliyo katika hali hatarishi na yaliyotengwa - katika kubuni, kupanga na kama inafaa, utekelezaji wa hatua za usimamizi, ikiwa ni pamoja na maeneo ya hifadhi, zinazoathiri chaguzi zao za kuendesha maisha. Mifumo shirikishi ya usimamizi, kama vile usimamizi shirikishi, lazima kukuzwa kwa mujibu wa sheria za Nchi

5.16 Nchi zinapaswa kuhakikisha uanzishwaji upya au kukuza matumizi ya mifumo iliyopo ya ufuatiliaji, udhibiti na uangalizi (MCS) unaoweza kutumika na kufaa kwa ajili ya uvuvi mdogo mdogo. Zinapaswa kusaidia mifumo hiyo, kuwashirikisha wavuvi wadogo wadogo kama inavyofaa na kukuza mipango shirikishi katika muktadha wa usimamizi shirikishi. Nchi zinapaswa kuhakikisha taratibu za ufuatiliaji na utekelezaji madhubuti wa kuepusha , kuzuia na kutokomeza aina zote za vitendo vilivyo kinyume cha sheria na / au uvuvi haribifu ulio na athari hasi juu ya mifumo ikolojia ya bahari na ya nchi kavu. Nchi lazima ziwe na jitihada za kuboresha usajili wa shughuli. Wavuvi wadogo wadogo wanapaswa kusaidia mifumo ya ufuatiliaji, udhibiti na uangalizi (MCS) na kutoa kwa mamlaka ya uvuvi, taarifa zinazohitajika kwa ajili ya usimamizi wa shughuli.

5.17 Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa wajibu na majukumu katika muktadha wa mipango ya usimamizi shirikishi wa pande husika na wadau zinafafanuliwa na kukubalika kupitia mchakato shirikishi unaosaidiwa na sheria. Wahusika wote wanawajibika kuchukua usimamizi wa majukumu waliyokubaliana. Jitihada zote zinapaswa kufanyika ili wavuvi wadogo wadogo wanawakilishwa katika vyama vya kitaalamu na vyombo vya uvuvi husika vya sehemu husika na nchi, na kushiriki kikamilifu katika kutoa maamuzi na michakato muhimu ya kuunda sera.

5.18. Nchi na washiriki katika uvuvi mdogo mdogo wanapaswa kuhamasisha na kusaidia jukumu na ushiriki wa wanaume na wanawake, iwe kushiriki katika shughuli za kabla ya mavuno, wakati wa mavuno au shughuli za baada ya mavuno, katika muktadha wa usimamizi shirikishi na katika uendelezaji uvuvi yakinifu , kuchangia maarifa yao maalum, mitazamo na mahitaji. Wahusika wote ni lazima kuangalia kwa makini haja ya kuhakikisha ushiriki sawa wa wanawake, kubuni hatua maalum ili kufikia lengo hili

5.19 Iwapo masuala yanayovuka mipaka ya nchi na masuala mengine kama hayo yapo, kwa mfano maji na rasilimali za uvuvi za pamoja, Nchi zinapaswa kufanya kazi kwa pamoja ili

kuhakikisha kuwa haki ya umiliki wa jumuiya za wavuvi wadogo wadogo zilizotolewa zinalindwa.

5.20 Nchi zinapaswa kuepuka sera na hatua za kifedha ambazo zinaweza kuchangia uvuvi kupita kiasi na hivyo, matumizi ya rasilimali ambayo yana madhara makubwa juu ya uvuvi mdogo mdogo

6. MAENDELEO YA JAMII, AJIRA NA KAZI ZA KUHESHIMIKA

6.1 Wahusika wote wanapaswa kufikiria mbinu kamilifu, za mfumo ikolojia na kijumla za usimamizi na maendeleo ya uvuvi mdogo mdogo ambayo itazingatia utata wa shughuli za kimaisha. Umakini utahitajika juu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ili kuhakikisha kuwa jamii ya wavuvi wadogo wadogo ina uwezo na inaweza kufurahia haki zao za kibinadamu.

6.2 Nchi zinapaswa kukuza uwekezaji katika maendeleo ya rasilimali watu kama vile afya, elimu, kusoma na kuandika ikiwemo elimu ya digitali na aina nyingine za ujuzi wa asili ya kiufundi ili kuzalisha ongezeko la thamani ya rasilimali za uvuvi ikiwa ni pamoja na uhamasishaji. Nchi inapaswa kuchukua hatua kwa lengo la kuendelea kuhakikisha kuwa walio katika jamii ya wavuvi wadogo wadogo na mafundi wanaweza kuwa na unafuu wa kuzifikia huduma hizi na zingine zilizo za muhimu kupitia hatua za ngazi ya kitaifa na chini ya hapo , ikiwa ni pamoja na makazi ya kutosha, usafi wa mazingira ulio safi na salama , maji safi na salama kwa ajili ya matumizi binafsi na ya majumbani , na vyanzo vya nishati. Upendeleo wa wanawake, wazawa, na makundi yaliyo katika hali hatarishi na waliotengwa - katika kutoa huduma na kuhakikisha kutobaguliwa na haki nyingine za binadamu - lazima zikubalike na kukuzwa ambako inapohitajika ili kuhakikisha manufaa sawa .

6.3 Nchi inapaswa kukuza ulindwaji wa usalama wa kijamii kwa wafanyakazi walio kwenye uvuvi mdogo mdogo. Wanapaswa kuzingatia uvuvi mdogo mdogo ulivyo na kutumia mipangilio ya usalama katika mlolongo mzima wa thamani.

6.4 Nchi inapaswa kusaidia uanzishwaji na upatikanaji wa huduma nyingine ambazo ni sahihi kwa jamii za wavuvi wadogo wadogo kuhusiana na, kwa mfano, mipangilio ya akiba, mikopo na bima, na mkazo maalum ukiwa juu ya kuhakikisha wanawake wanazifikia huduma hizo.

6.5 Nchi inapaswa kutambua kuwa shughuli zote zilizo katika mlolongo wa thamani wa uvuvi mdogo mdogo kuwa ni kazi za kiuchumi na kitaalamu - zote za kabla na baada ya mavuno; iwe katika mazingira ya maji au katika ardhi ; uliofanywa na wanaume ama wanawake. Shughuli zote zinapaswa kuchukuliwa kama: za muda, mara kwa mara na / au kwa ajili ya kujikimu. Fursa za maendeleo ya kitaalamu na kishirika lazima kukuzwa, hasa kwa wafanyakazi ambao wako katika vikundi vilivyo katika hali hatarishi wanaoshiriki kwenye shughuli za baada ya mavuno ya samaki na wanawake katika uvuvi mdogo mdogo.

6.6 Nchi inapaswa kukuza kazi za kuheshimika kwa wafanyakazi wote wa uvuvi mdogo mdogo, ikiwa ni pamoja na sekta rasmi na isiyo rasmi. Nchi inapaswa kujenga mazingira mwafaka ili kuhakikisha kuwa shughuli za uvuvi katika sekta rasmi na isiyo rasmi zinachukuliwa ili kuhakikisha uendelevu wa uvuvi mdogo mdogo kwa mujibu wa sheria za Nchi.

6.7 Nchi inapaswa kuchukua hatua za kuona kuwa haki ya wavuvi wadogo wadogo na wafanyakazi katika sekta ya uvuvi juu ya maisha bora na kufanya kazi kwa mujibu wa viwango vya haki za binadamu vya kitaifa na kimataifa vinaendela kufikiwa . Nchi lazima kujenga mazingira mazuri kwa maendeleo endelevu katika jamii za wavuvi wadogo wadogo. Nchi inapaswa kutekeleza sera bora za kiuchumi na zisizo za kibaguzi kwa ajili ya matumizi ya maeneo ya bahari, maziwa na mito na maeneo ya ardhi ili kuruhusu jamii za wavuvi wadogo wadogo na wazalishaji wengine wa chakula, hasa wanawake, kupata manufaa yanayostahili kutokana na kazi yao, mitaji na usimamizi, na kuhimiza uhifadhi na usimamizi endelevu ya maliasili

6.8 Nchi na wadau wengine wanapaswa kuunga mkono fursa mbadala za kujiongezea kipato zilizopo au kuanzisha , - nyongeza ya mapato kutokana na shughuli zinazohusiana na uvuvi - kwa jamii za wavuvi wadogo wadogo, kama inavyotakiwa na katika kusaidia matumizi endelevu ya rasilimali na maisha mseto. Kuna haja ya kutambuliwa na kunufaika jukumu la uvuvi mdogo mdogo katika uchumi wa ndani na kiunganishi cha sekta ndogo kwenye uchumi mpana. Jamii za wavuvi wadogo wadogo zinapaswa kunufaika sawa katika maendeleo kama vile ya utalii wa kijamii na wavugaji viumbe vya majini wadogo wadogo.

6.9 Nchi na wahusika wote lazima kuweka mazingira kwa wanaume na wanawake wa jamii za wavuvi wadogo wadogo kufanya shughuli zinazohusiana na uvuvi katika mazingira huru kutokana na uhalifu, vurugu, shughuli za uhalifu wa kimafia , uharamia, wizi, unyanyasaji wa kijinsia, rushwa na matumizi mabaya ya mamlaka. Wahusika wote ni lazima kuchukua hatua ambazo zitalenga katika kutokomeza vurugu na kulinda wanawake ambao hawana kinga na vurugu hizo katika jamii za wavuvi wadogo wadogo. Nchi inapaswa kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa waathirika wa unyanyasaji, dhuluma, nk, ikiwa ni pamoja na ndani ya kaya au jamii

6.10 Nchi na washiriki katika uvuvi mdogo mdogo , ikiwa ni pamoja na mamlaka za jadi na kimila, wanapaswa kuelewa, kutambua na kuheshimu nafasi ya wavuvi wahamiaji na wafanyakazi katika sekata ya uvuvi mdogo mdogo, kutokana na kwamba uhamiaji ni mikakati ya kawaida ya maisha katika uvuvi mdogo mdogo. Nchi na washiriki katika uvuvi mdogo mdogo wanapaswa kushirikiana ili kujenga mifumo sahihi kwa ajili ya kuruhusu ushirikiano wa haki na wa kutosha wa wahamiaji ambao hushiriki katika matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na wasio hujumu utawala na maendeleo ya uvuvi wa kijamii katika uvuvi mdogo mdogo kwa mujibu wa sheria za Nchi. Nchi zinapaswa kutambua umuhimu wa kuratibu miongoni mwa serikali za kitaifa husika kuhusu uhamiaji wa wavuvi na wafanyakazi katika uvuvi mdogo mdogo nje ya mipaka ya nchi. Sera na hatua za usimamizi zinapaswa kufanyiwa kazi kwa kushauriana na mashirika na taasisi za uvuvi mdogo mdogo.

6.11 Nchi inapaswa kutambua na kushughulikia visababishi na matokeo ya wavuvi kutembea na kuvuka mipaka ya nchi na kuchangia katika uelewa wa masuala kwenye mipaka ya nchi yanayoathiri uendelevu wa uvuvi mdogo mdogo.

6.13 Nchi zinapaswa kushughulikia masuala ya afya makazini na hali duni za kazi za wavuvi wote wadogo wadogo na wafanyakazi kwenye uvuvi kwa kuhakikisha kuwa zipo sheria muhimu na zinatekelezwa kwa mujibu wa sheria za nchi na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu na mikataba ya kimataifa ambayo Serikali ni mwanachama , kama vile Mkataba wa Kimtaifa wa Uchumi, Haki za Jamii na Utamaduni (ICESCR) na makubaliano husika ya Shirika la Kazi Duniani (ILO). Wahusika wote ni lazima kujitahidi kuhakikisha ushirikishwaji wa vipengele vya afya na usalama kama sehemu muhimu ya usimamizi wa uvuvi ikiwa ni pamoja na jitihada za maendeleo.

6.13 Nchi zinapaswa kutokomeza kazi za kulazimishwa, kuzuia utumwa wa madeni kwa wanawake, wanaume na watoto, na kuchukua hatua madhubuti za kulinda wavuvi na wafanyakazi katika uvuvi , ikiwa ni pamoja na wahamiaji, kwa matazamo wa kuondoa kabisa kazi za kulazimishwa katika uvuvi, ikiwa ni pamoja na uvuvi mdogo mdogo.

6.14 Nchi zinapaswa kutoa na kuwezesha kuzifikia huduma za shule na vituo vya elimu ili kukidhi mahitaji ya jamii za wavuvi wadogo wadogo na zitazowezesha upatikanaji wa ajira za maana kwa vijana, kuheshimu uchaguzi wao wa kazi na kutoa fursa sawa kwa wavulana wote na wasichana na vijana wanaume na wanawake

6.15 Washiriki katika uvuvi mdogo mdogo wanapaswa kutambua umuhimu wa ustawi wa watoto na elimu kwa ajili ya maisha ya baadaye ya watoto wenyewe na jamii kwa ujumla. Watoto wanatakiwa kwenda shule, kulindwa kutokana na unyanyasaji wowote na haki zao zote kuheshimiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Haki za Mtoto.

6.16 Wahusika wote ni lazima kutambua utata unaozingira masuala ya usalama baharini (katika uvuvi katika maziwa, mito na baharini) na sababu mbalimbali zilizopo nyuma ya upungufu wa usalama. Hii ni kwa shughuli zote za uvuvi. Nchi zinapaswa kuhakikisha uanzishwaji , utungwaji na utekelezaji wa sheria mwafaka za kitaifa ambazo ziko sawa na miongozo ya kimataifa ya Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) , Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Shirika la Kimataifa la Mabo ya Bahari (IMO) kwa ajili ya kazi katika uvuvi na usalama baharini katika uvuvi mdogo mdogo

6.17 Nchi zinapaswa kutambua kuwa usalama baharini ulioboreka, ambao ni pamoja na afya na usalama sehem za kazi , katika uvuvi mdogo mdogo (bara na baharini) utapatikana kupitia kuanzishwa na utekelezaji wa mikakati madhubuti na jumuishi ya kitaifa, na ushiriki wa wavuvi wenyewe na ukiwa na mambo ya kuratibiwa na kanda, kama inafaa. Kwa nyongeza , usalama baharini wa wavuvi wadogo wadogo unapaswa pia kujumuishwa katika usimamizi wa jumla wa uvuvi. Nchi inapaswa kusaidia , pamoja na mambo mengine, kuwepo kwa utoaji wa taarifa, kuwepo kwa mipango ya utoaji wa elimu ya ufahamu wa usalama baharini na kuanzishwa kwa

sheria sahihi kwa ajili ya usalama baharini katika uvuvi mdogo mdogo. Jukumu la taasisi zilizopo na miundo ya kijamii kwa ajili ya kuongeza kutii, ukusanyaji wa takwimu, mafunzo na mwamko, na shughuli za utafutaji na uokoaji zinapaswa kutambuliwa katika mchakato huu. Nchi inapaswa kukuza upatikanaji wa habari na mifumo ya kujua maeneo ya dharura kwa ajili ya kuokoa vyombo vidogo vidogo katika bahari

6.18 Wahusika wote ni lazima kulinda haki za binadamu na utu wa wadau kwenye uvuvi mdogo mdogo katika hali ya uvamizi ili kuwaruhusu kuendelea na maisha yao ya kijadi, kuwepo na upatikanaji wa sehemu za uvuvi za kimila na kuhifadhi utamaduni wao na njia ya maisha. Ni lazima kuwezesha ushiriki wao katika kutoa maamuzi juu ya masuala yanayowahusu.

Kwa kuzingatia mwongozo wa Hiari kwa ajili ya Jukumu la Utawala wa Umiliki Ardhi, Uvuvi na Misitu katika Muktadha wa Usalama wa Chakula wa Taifa [ikiwa ni pamoja na kifungu cha 25], wahusika wote ni lazima kulinda haki za binadamu na utu wa wadau kwenye uvuvi mdogo mdogo wakati wa migogoro ya kivita, kwa mujibu wa sheria za kibinadamu za kimataifa ili kuwaruhusu kuendelea na maisha yao ya kijadi, kuwepo na upatikanaji wa sehemu za uvuvi za kimila na kuhifadhi utamaduni wao na njia ya maisha. Ni lazima kuwezesha ushiriki wao katika kutoa maamuzi juu ya mambo ambayo yanawaathiri.

7. MINYORORO YA THAMANI, BAADA YA MAVUNO NA BIASHARA

7.1 Wahusika wote ni lazima kutambua jukumu kubwa ambalo sekta ndogo ya uvuvi mdogo mdogo ya baada ya mavuno na washiriki wake wanavyochangia katika mlolongo wa thamani. Wahusika wote wanapaswa kuhakikisha kuwa washiriki wote wa shughuli za baada ya mavuvi ni sehemu ya wafanya maamuzi muhimu, na kutambua kuwa wakati mwengine huwa hakuna uwiano wa usawa katika uhusiano wa mamlaka kati ya washiriki katika mlolongo wa thamani na kwamba makundi yaliyo katika hali hatarishi na waliotengwa yatahitaji msaada maalum.

7.2 Wahusika wote ni lazima kutambua jukumu la wanawake wanavochangia katika sekta ndogo ya shughuli za baada ya mavuvi na ni lazima wasaidie kuboresha ili kuwezesha ushiriki wa wanawake katika kazi. Nchi inapaswa kuhakikisha kuwa huduma sahihi kwa wanawake zinapatikana kama inavyotakiwa ili kuwawezesha wanawake kurejesha na kuimarisha maisha yao katika sekta ndogo ya shughuli za baada ya mavuvi

7.3 Nchi zinapaswa kuendeleza, kutoa na kuwezesha uwekezaji katika miundombinu sahihi, miundo ya shirika na kujenga uwezo ili kusaidia shughuli za sekta ndogo ya uvuvi mdogo mdogo baada ya mavuvi, katika kuzalisha bidhaa bora na salama za samaki, kwa kuuza nje na masoko ya ndani, katika namna ya kuwajibika na endelevu

7.4 Nchi na washirika wa maendeleo wanapaswa kutambua aina ya vyama vya kijadi vya wavuvi na wafanyakazi katika uvuvi na kuzijengea uwezo wa kutosha katika hatua zote za mlolongo wa thamani ili kuongeza mapato yao na usalama wa kimaisha kwa mujibu wa sheria za Nchi. Ipasavyo, pia kuna haja ya kuwepo msaada kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza ushirika,

mashirika ya kitaalamu katika sekta ya wavuvi wadogo wadogo na miundo ya shirika nyingine , ikiwa ni pamoja na taratibu za masoko,kwa mfano mnada kama inafaa.

3 Hizi ni ikiwa pamoja na mambo mengine., Kanuni za Usalama kwa Wavuvi na Vyombo vya Uvuvi (tangu zifanyiwe marekebisho) ya 1968, FAO / ILO / IMO Miongozo wa Hiari kwa ajili ya usanifu, Ujenzi na Vifaa vya Vyombo vya Uvuvi Vidogo Vidogo ya 1980, na Mapendekezo ya Usalama ya vyombo vya Uvuvi vya urefu wa Mita Chini ya 12 vilivyo..... na vyombo vya Uvuvi visivyo Undecked ya 2010.

7.5 Washirika wote ni lazima kuepuka upotevu na hasara baada ya mavuno na kutafuta njia za kutengeneza ongezeko la thamani, kwa kutumia teknolojia za kijadi zenye gharama nafuu zilizopo , ubunifu wa ndani na uhamishwaji wa teknolojia zilizo sahihi kiutamaduni. Matendo endelevu kimazingira ndani ya mbinu za mfumo ikolojia lazima kukuzwa, kuzuia, kwa mfano, upotevu wa pembejeo (maji, kuni, nk) katika utunzaji na usindikaji wa samaki wa wavuvi wadogo wadogo .

7.6 Nchi zinapaswa kuwezesha kufikika kwenye masoko ya ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa na kukuza usawa na usio wa kibaguzi wa biashara kwa ajili ya bidhaa za uvuvi mdogo mdogo . Nchi zinapaswa kufanya kazi kwa pamoja ili kuanzisha kanuni za biashara na taratibu ambazo hasa zinasaidia biashara za bidhaa za wavuvi wadogo wadogo katika kanda kwa kuzingatia mikataba chini ya Shirika la Biashara Duniani (WTO), kwa kuzingatia haki na wajibu wa wanachama wa WTO pale inapobidi

7.7. Nchi zinapaswa kufikiria athari za biashara ya kimataifa kwa samaki na bidhaa za samaki na ushirikiano juu ya wavuvi wadogo wadogo wa ndani, wafanyakazi na jamii zao. Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa uendelezaji wa biashara ya kimataifa wa samaki na uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje hauathiri mahitaji ya lishe ya watu ambao samaki ni muhimu kwa lishe bora, afya zao na ustawi na ambao vyanzo vingine vya chakula vya kulinganishwa bado havijapatikana au kuvimudu.

7.8 Nchi, na washiriki katika uvuvi mdogo mdogo na wengineo kwenye mlolongo wa thamani wanapaswa kutambua kuwa manufaa yanayotokana na biashara ya kimataifa yanapaswa kugawia sawa . Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa mifumo fanisi ya usimamizi wa uvuvi ipo ili kuzuia uvuvi kupita uwezo unaoendeshwa kwa mahitaji ya soko ambao unaweza kutishia uendelevu wa rasilimali za uvuvi, usalama wa chakula na lishe. Mifumo hiyo ya usimamizi wa uvuvi ni pamoja na matendo ya kuwajibika kwenye shughuli za baada ya mavuno , sera na hatua ili kuwezesha mapato ya mauzo ya nje yanawanufaisha wavuvi wadogo wadogo na wengine kwa njia ya usawa katika mololongo wa thamani wote.

7.10 Nchi zinapaswa kupitisha sera na taratibu, ikiwa ni pamoja na tathmini ya kimazingira, kijamii na mengine muhimu, ili kuhakikisha kwamba athari mbaya za biashara ya kimataifa juu ya mazingira, utamaduni wa wavuvi wadogo wadogo, shughuli za maisha na mahitaji maalum

kuhusiana na usalama wa chakula yanapata ufumbuzi sawa . Mashauriano na wadau yanapaswa kuwa sehemu ya sera na taratibu hizi.

7.10 Nchi zinapaswa kuwezesha upatikanaji wa taarifa zote muhimu za masoko na biashara kwa wadau katika mlolongo wa thamani wa uvuvi mdogo mdogo. Wadau katika uvuvi mdogo mdogo ni lazima kupata kwa wakati taarifa sahihi ya soko ili kuwasaidia kuendana na mabadiliko ya hali ya soko. Kujenga uwezo pia kunahitajika ili wadau wote wa uvuvi mdogo mdogo na hasa wanawake na makundi yaliyo katika hali hatarishi na waliotengwa wanaweza kukabiliana na kunufaika kwa usawa kutokana na , fursa za mwenendo wa soko la kimataifa na hali ya ndani wakati huo huo kupunguza uwezekano wa athari yoyote hasi

8 USAWA WA KIJINSIA

8.1 Washiriki wote wanapaswa kutambua kwamba kufikia usawa wa kijinsia kunahitaji juhudi za pamoja na kwamba kuingiza masuala ya jinsia inapaswa kuwa sehemu muhimu ya mikakati yote ya maendeleo ya uvuvi mdogo mdogo. Ili mikakati hii kufikia usawa wa kijinsia inahitaji mbinu mbalimbali katika mazingira tofauti ya kitamaduni na inapaswa kutoa changamoto kwa matendo ambayo ni ya kibaguzi dhidi ya wanawake.

8.2 Nchi ni lazima kuzingatia majukumu yao chini ya sheria za kimataifa za haki za binadamu na kutekeleza vyombo husika ambayo wao ni wanachama, ikiwa ni pamoja na mambo mengine. CEDAW, na kuzingatia Azimio la Beijing na Hatua zake. Nchi lazima kufanya jitihada za kupata ushiriki wa wanawake sawa katika mchakato wa kufanya maamuzi ya sera zinazolenga uvuvi mdogo mdogo. Nchi inapaswa kuchukua hatua maalum za kushughulikia ubaguzi dhidi ya wanawake, wakati ikiwa inajenga mazingira kwa ajili ya asasi za kiraia, hasa kwa wafanyakazi wanawake na mashirika yao, kushiriki katika ufuatiliaji wa utekelezaji wake. Wanawake wanapaswa kuhamasishwa kushiriki katika mashirika ya uvuvi, na msaada husika wa maendeleo wa shirika inapaswa kutolewa.

8.3 Nchi zianzishe sera na sheria ili kufikia usawa wa kijinsia na kama inafaa, kuchukua sheria, sera na hatua ambazo hazilingani na usawa wa kijinsia, kwa kuzingatia masuala ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Nchi zinapaswa kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza hatua kwa ajili ya kufikia usawa wa kijinsia na pamoja na mengine kuajiri wanaume na wanawake kama wataalamu wa ugani na kuhakikisha kwamba wanaume na wanawake wana haki sawa ya kupata ugani na huduma za kiufundi, ikiwa ni pamoja na msaada wa kisheria kuhusiana na uvuvi. Washiriki wote ni lazima kushirikiana kuanzisha mifumo inayofanya kazi ya kupima ili kutathmini athari za sheria, sera na hatua kwa ajili ya kuboresha hali ya wanawake na kufikia usawa wa kijinsia

8.4 Wahusika wote ni lazima kuhimiza kuanzishwa kwa teknolojia bora ya muhimu na sahihi kwa kazi za wanawake katika uvuvi mdogo mdogo.

9 HATARI ZA MAAFA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI

9.1 Nchi zinapaswa kutambua kwamba kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, ikiwa ni pamoja na katika muktadha wa uvuvi mdogo mdogo endelevu, inahitaji hatua za haraka na kabambe, kwa mujibu wa malengo, kanuni na masharti ya Umoja wa Nchi kuhusu TabiaNchi (UNFCCC), kwa kuzingatia matokeo ya waraka wa Mkutano wa Umoja wa Nchi kuhusu maendeleo endelevu (Rio + 20) 'Hali ya baadaye tunayotaka'

9.2 Wahusika wote ni lazima kutambua na kuzingatia athari tofauti ya mabadiliko ya tabia nchi yanayosababishwa na majanga ya asili na binadamu juu ya uvuvi mdogo mdogo. Nchi zinatakiwa kubuni sera na mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya nchi katika uvuvi, hasa mikakati maalum kwa ajili ya kukubiliana na kukabiliana na hali hiyo , na pia kwa ajili ya kujenga uwezo wa kukabiliana , kwa kushauriana kikamilifu na jamii za wavuvi ikiwa ni pamoja na wazawa, wanaume na wanawake, kutoa hasa kipaumbele kwa makundi yaliyo katika hali hatarishi na waliotengwa . Misaada maalumu itolewe kwa jamii za wavuvi wadogo wadogo wanaoishi katika visiwa vidogo ambako mabadiliko ya tabia nchi yanaweza kuwa na athari maalum kwa ajili ya usalama wa chakula, lishe, makazi na maisha.

9.3 Wahusika wote wanapaswa kutambua umuhimu wa njia jumuishi na za kamilifu , ikiwa ni pamoja ushirikiano wa sekta mtambuka, ili kukabiliana na hatari ya maafa na mabadiliko ya tabia nchi katika uvuvi mdogo mdogo. Nchi na washiriki wengine wanapaswa kuchukua hatua kushughulikia masuala kama vile uchafuzi wa mazingira, mmomonyoko wa fukwe na uharibifu wa makaziya viumbe maeneo ya pwani kutokana na mambo yanayosababishwa na kibinadamu yasiyohusiana na uvuvi. Wasiwasi kama huo hudhoofisha shughuli za kimaisha za jamii ya wavuvi pamoja na uwezo wao wa kukabiliana na uwezekano wa athari za mabadiliko ya tabia nchi.

9.4 Nchi zinapaswa kufikiria kusaidia jamii za wavuvi wadogo wadogo walioathirika na mabadiliko ya tabia nchi au majanga ya asili na yanayosababishwa na binadamu, ikiwa ni pamoja na kupitia kukubaliana , kukabiliana na mipango ya misaada, ambapo inafaa

9.5 Inapotokea majanga ni yale yanayosababishwa na binadamu kuathiri uvuvi mdogo mdogo, wahusika wote wanapaswa kuwajibika

9.6 Wahusika wote wanapaswa kuzingatia mabadiliko ya tabia nchi na majanga yavyoweza kuathiri shughuli za sekata za baada ya mavuno na biashara katika hali ya mabadiliko katika aina na wingi wa samaki , ubora wa samaki na mda wa kukaa kabla ya kuliwa, na athari kuhusiana na masoko. Nchi zinapaswa kutoa msaada kwa wadau wa uvuvi mdogo mdogo kwa kuzingatia hatua za marekebisho ili kupunguza athari mbaya. Wakati teknolojia mpya zinapoanzishwa , zinahitajika kuwa rahisi kubadilika na kukubaliana na mabadiliko ya baadaye katika jamii ya samaki, bidhaa na masoko, na mabadiliko ya hali ya hewa.

9.7 Nchi zinapaswa kuelewa jinsi maandalizi ya kukabilina na dharura na majanga yanavyohuisiana katika uvuvi mdogo mdogo na kutumia dhana ya muendelezo wa utoaji misaada . Kuna haja ya kuzingatia malengo ya maendeleo ya muda mrefu katika mlolongo wa dharura, ikiwa ni pamoja na katika awamu ya misaada ya haraka, ukarabati, ujenzi na kufufua ni lazima kuweko na vitendo vya kupunguza hali ya kuwa katika hatari ya vitisho vya baadaye vinavyoweza kutokea. Dhana ya 'kuijenga upya vizuri' inapaswa kutekelezwa katika kukabiliana na matukio ya maafa na ukarabati

9.8 Wahusika wote wanapaswa kuendeleza wajibu wa uvuvi mdogo mdogo katika jitihada kuhusiana na mabadiliko ya tabia nchi na inawalazimu kuhimiza na kusaidia ufanisi wa nishati katika sekata, ikiwa ni pamoja na mlolongo wa thamani mzima wa uvuvi, baada ya mavuvi, masoko na usambazaji.

9.9 Nchi zinapaswa kufikiria kama inafaa upatikanaji kwa uwazi kwa jamii za wavuvi wadogo wadogo wa fedha za kukabiliana, vifaa vya na / au teknolojia sahihi inayoendana na utamaduni kwa ajili ya mabadiliko ya tabia nchi .

SEHEMU 3: KUHAKIKISHA KUWEPO KWA MAZINGIRA WEZESHAJI NA KUSAIDIA UTEKELEZAJI

10. SERA MSHIKAMANO, URATIBU WA TAASISI NA USHIRIKIANO

10.1 Nchi zinapaswa kutambua haja na kufanyia kazi katika kuelekea mshikamano wa sera kwa kuzingatia, pamoja na mambo mengine: sheria ya nchi; sheria za kimataifa za haki za binadamu; vyombo vingine vya kimataifa, ikiwa ni pamoja na zile zinazohusiana na wenyeji; sera za maendeleo ya kiuchumi; nishati, elimu, afya na sera za vijijini; kulinda mazingira; sera za usalama wa chakula na lishe; sera za kazi na ajira; sera za biashara; usimamizi wa hatari za majanga (DRM) na sera za mabadiliko ya tabia nchi (CCA); mpango wa kuyafikia maeneo ya uvuvi ; na sera nyingine za uvuvi , mipango, hatua na uwekezaji ili kukuza maendeleo ya kiujumla katika jamii za wavuvi wadogo wadogo. Tahadhari maalumu inapaswa kupewa katika kuhakikisha usawa wa kijinsia

10.2 Nchi ni lazima, kama inafaa, kuanzisha na kutumia njia za mipango ya maeneo , ikiwa ni pamoja na mipango ya maeneo ya nchi kavu na baharini , ambayo inazingatia maslahi na nafasi ya uvuvi mdogo mdogo katika usimamizi kamilifu wa ukanda wa pwani . Kupitia mashauriano, ushiriki na kujitangaza, sera sensitive juu ya jinsia na sheria juu ya mipango ya maeneo zinapaswa ziundwe kama inafaa. Iwapo inafaa , mifumo rasmi ya mipango inapaswa kufikiria njia za mipango na uendelezeja wa maeneo ya kiutawala inayotumiwa na wavuvi wadogo wadogo na jamii nyingine iliyo na mifumo ya kimila ya umiliki, na maamuzi ndani ya jamii hizo

10.3 Nchi ni lazima kuzichukua hatua za sera maalum ili kuhakikisha kuoanisha sera zinazoathiri hali nzuri ya bahari , maziwa na mito na mfumo ikolojia na kuhakikisha kuwa uvuvi, kilimo na

sera nyingine za maliasili kwa pamoja zinaimarisha shughuli za kimaisha zinazohusiana kutokana na sekta hizi.

10.4 Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa sera ya uvuvi hutoa muono wa muda mrefu kwa ajili ya uvuvi mdogo mdogo endelevu na kutokomeza njaa na umaskini, kwa kutumia njia ya mfumo ikolojia. Mfumo wa sera ya ujumla kwa ajili ya uvuvi lazima ulingane na muono wa muda mrefu na mfumo wa sera kwa ajili ya uvuvi mdogo mdogo na haki za binadamu, kuweka kipaumbele maalum kwa watu wanaoishi katika hali hatarishi na waliotengwa.

10.5 Nchi zinatakiwa kuandaa na kukuza miundo ya kitaasisi na viunganishi - ikiwa ni pamoja na uhusiano wa ndani-ya taifa -ya kikanda-kimataifa na mitandao - muhimu kwa ajili ya kufikia mshikamano wa sera, ushirikiano wa sekta mtambuka na utekelezaji wa kiujumla wa njia za mfumo wa kiikolojia katika sekta ya uvuvi. Wakati huo huo, kuna haja ya majukumu ya wazi na kuwe na sehemu inayojulikana ya kuwasiliana katika mamlaka za serikali na mashirika kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo.

10.6 Wadau wa uvuvi mdogo mdogo wanapaswa kukuza ushirikiano kati ya vyama vyao vya kitaaluma, ikiwa ni pamoja na ushirika wa wavuvi na asasi za kiraia. Wanapaswa kuanzisha mitandao na majukwaa kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na habari na kuwezesha ushiriki wao katika michakato ya maamuzi muhimu ya sera zinazohusu jamii ya wavuvi wadogo wadogo

10.7 Nchi zinapaswa kutambua, na kukuza kama inafaa, miundo ya utawala wa ndani ambayo inaweza kuchangia usimamizi bora wa uvuvi mdogo mdogo, kwa kuzingatia njia ya mfumo ikolojia na kwa mujibu wa sheria za nchi.

10.8 Nchi ni lazima kukuza ushirikiano wa kimataifa, kikanda ulioimarika katika kupata uhakika wa uvuvi mdogo mdogo endelevu . Nchi , ikiwa ni pamoja na mashirika ya kimataifa, kikanda , kama inafaa, inapaswa kusaidia kujenga uwezo ili kuboresha uelewa wa uvuvi wadogo wadogo na kusaidia sekata ndogo za uvuvi katika masuala ambayo yanahitaji ushirikiano wa kikanda au kimataifa , ikiwa ni pamoja na uhamisho sahihi wa teknolojia inayokubalika

11. TAARIFA, UTAFITI NA MAWASILIANO

11.1 Nchi ni lazima zianzishe mfumo wa kukusanya takwimu za uvuvi, ikiwa ni pamoja na takwimu muhimu za kiikolojia , kijamii, kiutamaduni na kiuchumi kwa ajili ya kufanya maamuzi juu ya usimamizi endelevu wa uvuvi mdogo mdogo kwa lengo la kuhakikisha uendelevu wa mfumo wa ikolojia , ikiwa ni pamoja na samaki, katika hali ya uwazi. Juhudi zinapaswa kufanyika pia kuzalisha takwimu katika takwimu za serikali za jinsia zilizogawanywa, ikiwa ni pamoja na takwimu za kuruhusu kuwepo na ufahamu bora wa kujulikana juu ya umuhimu wa uvuvi mdogo mdogo na sehemu zake tofauti, ikiwa ni pamoja na masuala ya kijamii na kiuchumi.

11.2 Wadau wote na jamii ya uvuvi mdogo mdogo inapaswa kutambua umuhimu wa mawasiliano na habari, ambayo ni muhimu kwa ufanisi wa maamuzi

11.3 Nchi ni lazima kufanya jitihada za kuzuia rushwa, hasa kwa njia ya kuongeza uwazi, kuwawajibisha wafanya maamuzi, na kuhakikisha kwamba maamuzi yasiyo na upendeleo yanatolewa kwa haraka kupitia ushiriki na mawasiliano sahihi na jamii za wavuvi wadogo wadogo,

11.4 Wahusika wote wanapaswa kutambua jamii za wavuvi wadogo wadogo kama wamiliki, watoa na wapokezi wa maarifa. Ni muhimu hasa kuelewa haja ya jamii za wavuvi wadogo wadogo na mashirika yao kupata habari sahihi ili kusaidia kukabiliana na matatizo yaliyopo na kuwapa uwezo wa kuboresha shughuli za kimaisha zao. Mahitaji haya ya habari hutegemea masuala ya sasa yanayokabili jamii na yanayohusiana na masuala ya kibaolojia, kisheria, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ya uvuvi na shughuli za kimaisha.

11.5 Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa taarifa muhimu kwa ajili ya uvuvi mdogo mdogo yakinifu na maendeleo endelevu zinapatikana, ikiwa ni pamoja na juu ya uvuvi haramu, usioripotiwa na usiosimamiwa. Ni lazima uhusiane pamoja na mambo mengine na hatari za maafa, mabadiliko ya tabia nchi , shughuli za kimaisha na usalama wa chakula kwa kuzingatia hali ya makundi yaliyo katika hali hatarishi na yaliyotengwa . Mifumo ya taarifa yenye mahitaji ya takwimu za chini iundwe kwa ajili ya hali masikini za takwimu.

11.6 Wahusika wote wanapaswa kuhakikisha kuwa maarifa, utamaduni, mila na desturi za jamii za wavuvi wadogo wadogo, ikiwa ni pamoja na wazawa, zinatambuliwa na kama inafaa, kusaidiwa , na kwamba zinajulisha utawala wa serikali na michakato ya maendeleo endelevu. Maarifa maalum ya wavuvi wanawake na wafanyakazi katika uvuvi ni lazima kutambuliwa na kuungwa mkono. Nchi zinapaswa kuchunguza na kuweka kumbukumbu za maarifa ya uvuvi wa jadi na teknolojia ili kutathmini matumizi yake kwenye uhifadhi , usimamizi na maendeleo ya uvuvi endelevu.

11.7 Nchi na wahusika wote muhimu wanapaswa kutoa msaada kwa jamii za wavuvi wadogo wadogo, hasa kwa wazawa, wanawake na wale wanaotegemea uvuvi kwa ajili ya kujikimu, ikiwa ni pamoja na, kama inafaa, msaada wa kiufundi na kifedha ili kupanga, kudumisha, kubadilishana na kuboresha maarifa ya jadi ya rasilimali za majini na mbinu za uvuvi, na kuboresha maarifa katika mfumo ikolojia ya majini.

11.8 Wahusika wote ni lazima kukuza upatikanaji, mtiririko na kubadilishana habari, ikiwa ni pamoja na juu ya rasilimali za majini zilizoko kati ya mipaka, kwa njia ya uanzishwaji au matumizi ya majukwaa sahihi yaliyopo na mitandao katika jamii, ngazi ya kitaifa na kikanda, ikiwa ni pamoja na mtiririko wa habari pande zote mbili. Kwa kuzingatia vipimo vya kijamii na kiutamaduni, mbinu sahihi , zana na vyombo vya habari vinapaswa kutumika kwa ajili ya mawasiliano na kujenga uwezo wa jamii za wavuvi wadogo wadogo.

11.9 Nchi na wahusika wote ni lazima, kwa kiasi iwezekanavyo, kuhakikisha kuwa fedha kwa ajili ya utafiti juu ya uvuvi mdogo mdogo zipo za kutosha, na ushirikiano na ushirikishwaji wa ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na utafiti ni lazima uhamasishwe. Nchi na wahusika wengine ni lazima kufanya jitihada ili kuunganisha maarifa ya utafiti huu katika michakato yao ya kufanya maamuzi. Mashirika ya utafiti na taasisi zinapaswa kusaidia kujenga uwezo wa kutoa nafasi ya jumuiya za wavuvi wadogo wadogo kushiriki katika utafiti na katika matumizi ya matokeo ya utafiti. Ni lazima kukubaliana vipaumbele vya utafiti kupitia mchakato wa mashauriano unaolenga juu ya jukumu la uvuvi mdogo mdogo katika matumizi endelevu ya rasilimali, usalama wa chakula na lishe, kuondoa umaskini, na maendeleo yenye usawa, ikiwa ni pamoja na masuala ya usimamizi wa hatari za majanga na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi (DRM na CCA).

11.10 Nchi na wahusika wengine muhimu ni lazima kukuza utafiti katika mazingira ya kazi, ikiwa ni pamoja na wavuvi wahamiaji na wafanyakazi katika uvuvi , afya, elimu, utoaji wa maamuzi, nk katika muktadha wa mahusiano ya jinsia, ili kujulisha mikakati ya kuhakikisha kuwepo kwa manufaa yaliyosawa kwa wanaume na wanawake katika uvuvi. Jitihada za kuingiza masuala ya jinsia zinapaswa kuwa ni pamoja na matumizi ya uchambuzi wa kijinsia katika awamu ya kupanga sera, mipango na miradi kwa ajili ya uvuvi mdogo mdogo ili kubuni hatua zinazojali jinsia. Viashiria vinavyozigatia jinsia vitumike kufuatilia na kushughulikia ukosefu wa usawa wa kijinsia na kufahamu jinsi hatua zimechangia kuelekea mabadiliko ya kijamii.

11.11 Kwa kutambua umuhimu wa uvuvi mdogo mdogo katika uzalishaji wa mazao ya bahari, Nchi na wahusika wengine ni lazima kukuza ulaji wa samaki na bidhaa za uvuvi ndani ya programu za elimu ya walaji ili kuongeza ufahamu wa manufaa ya lishe ya kula samaki na kutoa elimu juu ya jinsi ya kutathmini ubora wa samaki na bidhaa za uvuvi.

12. KUJENGA UWEZO

12.1 Nchi na wahusika wote ni lazima kuimarisha uwezo wa jamii za wavuvi wadogo wadogo ili kuwawezesha kushiriki katika mchakato wa utoaji wa maamuzi. Kwa sababu hii, ni lazima kuhakikisha kwamba upana na wingi wa sekta ya uvuvi mdogo mdogo katika mlolongo mzima wa thamani unawakilishwa kisawasawa kupitia uundwaji miundo wakilishi, halali, na ya kidemokrasia . Kipaumbele maalum kinatakiwa kupewa umuhimu kwa haja ya kufanya kazi kuelekea ushiriki sawa wa wanawake katika miundo hiyo. Pale inapobidi na ni lazima, nafasi tofauti na taratibu zinapaswa kutolewa ili kuwawezesha wanawake kuandaa wenyewe katika ngazi mbalimbali bila kuingiliwa masuala fulani yaliyo na umuhimu kwao.

12.2 Nchi na wadau wengine wanapaswa kujenga uwezo, kwa mfano kupitia programu za maendeleo, kuruhusu uvuvi mdogo mdogo kunufaika na fursa za masoko.

12.3 Wahusika wote wanapaswa kutambua kwamba kujenga uwezo juu ya maarifa na ujuzi uliopo uwe wa mchakato wa njia mbili wa kuhamisha maarifa, kutoa njia za kujifunza rahisi na kufaa ili kukidhi mahitaji ya watu binafsi, ikiwa ni pamoja na wanaume na wanawake na

makundi ya yaliyo katika hali hatarishi na waliotengwa . Aidha, kujenga uwezo ni pamoja na ujenzi wa uwezo wa kuhimili na uwezo wa kuishi na mabadiliko ya jamii za wavuvi wadogo wadogo katika uhusiano na usimamizi wa hatari za majanga na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi.

12.4 Mamlaka za Serikali na vyombo katika ngazi zote zinapaswa kufanya kazi ya kuendeleza maarifa na ujuzi wa kusaidia maendeleo endelevu ya uvuvi mdogo mdogo na mipango ya usimamizi shirikishi yenye mafanikio, kama inafaa. Umakini hasa utolewe kwenye miundo ya serikali iliyogatuliwa moja kwa moja inayoshiriki katika michakato ya utawala na maendeleo pamoja na jumuiya za wavuvi wadogo wadogo, ikiwa ni pamoja na eneo la utafiti.

13. KUSAIDIA UTEKELEZAJI NA UFUATILIAJI

13.1 Wahusika wote wanahamasishwa kutekeleza Miongozo hii kwa mujibu wa vipaumbele vya Taifa na mazingira yaliyopo.

13.2 Nchi na wahusika wengine wote wanapaswa kukuza ufanisi wa misaada na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali fedha. Washirika wa maendeleo, Mashirika maalumu ya Umoja wa Mataifa, na mashirika ya kikanda yanahamasishwa kuunga mkono juhudi za hiari na Nchi kutekeleza Miongozo hii, ikiwa ni pamoja na kupitia ushirikiano wa Kusini-Kusini. Msaada huo ni pamoja na ushirikiano wa kiufundi, msaada wa kifedha, kujenga uwezo wa kitaasisi, kubadilishana maarifa na kubadilishana uzoefu, msaada katika kutengeneza sera za kitaifa za wavuvi wadogo wadogo na uhamisho wa teknolojia

13.3 Nchi na wahusika wote wanapaswa kufanya kazi pamoja ili kujenga uelewa wa Miongozo, pia na kusambaza tafsiri rahisi na matoleo kwa manufaa ya wale wanaofanya kazi katika uvuvi mdogo mdogo. Nchi na wahusika wengine wote wanapaswa kutengeneza seti maalum ya vifaa juu ya jinsia ili kupata usambazaji mzuri wa habari juu ya jinsia na jukumu la wanawake katika uvuvi mdogo mdogo na kuonyesha hatua ambazo zinahitajika kuchukuliwa ili kuboresha hali ya wanawake na kazi zao

13.4 Nchi yanapaswa kutambua umuhimu wa mifumo ya ufuatiliaji ili kuruhusu taasisi zao kutathmini maendeleo kuelekea utekelezaji wa malengo na mapendekezo katika miongozo hii. Ni lazima kuwepo tathmini ya athari kwenye kufurahia utambuzi taratibu wa haki ya kupata chakula cha kutosha katika muktadha wa usalama wa chakula kitaifa na juu ya kuondoa umaskini . Ni lazima kuwepo kwa taratibu za kuruhusu mrejesho wa matokeo ya ufuatiliaji katika uundaji na utekelezaji wa sera. Jinsia lazima kuzingatiwa katika ufuatiliaji kwa kutumia njia sensitive za kijinsia , viashiria na takwimu . Nchi na wahusika wote ni lazima kufafanua mbinu za tathmini shirikishi zinazoruhusu uelewa mzuri na uwekaji kumbukumbu wa nyaraka za mchango wa kweli wa uvuvi mdogo mdogo kwenye usimamizi endelevu wa rasilimali kwa ajili ya usalama wa chakula na kuondoa umaskini ikiwa ni pamoja na wanaume na wanawake

13.5 Nchi inapaswa kuwezesha kuanzishwa kwa majukwaa ngazi ya taifa, na uwakilishi kisekta mtambuka na kwa uwakilishi mkubwa wa asasi za kiraia, kusimamia utekelezaji wa miongozo, kama inafaa. Wawakilishi halali wa jumuiya za wavuvi wadogo wadogo wanapaswa kushiriki katika kuanzisha na matumizi ya mikakati ya utekelezaji kwa ajili ya miongozo na katika kufuatilia.

13.6 Shirika la Chakula na Kilimo FAO lazima kukuza na kusaidia maendeleo ya Programu ya Msaada wa Ulimwengu , na mipango ya utekelezaji ya kikanda ya kusaidia utekelezaji wa Miongozo hii